

Neno La Jumuiya

Hakika mirathi ya Ahlul-Bait ambayo imehifadhiwa na madhehebu yao na wafuasi wao dhidi ya upotovu inaonyesha madhehebu iliyokusanya aina mbalimbali za taaluma za kiislamu.

Kambi hii imeweza kulea nafsi mbalimbali zilizo tayari kunywa kutoka kwenye chemchemu hiyo, na kuupa umma wa kiislamu Wanachuoni wakubwa wenye kufuata nyayo za ujumbe wa Ahlul-Bait.

Wanachuoni waliyokusanya vidodosa na maswali mbalimbali ya madhehebu na mitazamo tofauti ya kifikiria kuanzia ndani ya desturi za kiislamu hadi nje ya desturi hizo, huku wao wakitoa majibu na utatuzi makini juu ya maswali hayo ndani ya karne zote.

Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait imefanya hima kutetea tukufu za ujumbe wa Uislamu na ukweli wake ambao umechafuliwa na makundi, madhehebu na wanaharakati mbalimbali wenye chuki na Uislamu.

Jumuiya imefuata nyayo za Ahlul-Bait na za wafuasi wa madhehebu yao njema ambayo imefanya hima kujibu madai yenye kuendelea na daima ika-jaribu kubaki ndani ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachohita-jika ndani ya kila zama.

Hakika uzoefu ambao umehifadhiwa ndani ya vitabu vya wanachuoni wa madhehebu ya Ahlul-Bait katika dhamira hii ni wa aina ya pekee, kwa sababu una akiba ya kielimu inayotegemea akili na hoja, huku ukijiepusha na matamano na upendeleo uliokatazwa.

Unazungumza na wasomi na wanafikra wenye fani maalumu, mazungumzo ambayo yanakubalika kiakili na yanapokewa na maumbile yaliyo sala-ma.

Jaribio hili la Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait limekuja kuwapa watafu-ta ukweli hatua mpya ya uzoefu wa thamani katika ulingo wa mazungumzo na maswali na kujibu hoja za utata zilizotolewa zama zilizopita au zina-zotolewa leo kwa njia ya Tovuti, na hasa kwa kupewa nguvu na baadhi ya duru zenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ikijiepusha na uchochezi uliokatazwa, na ni yenye kuhangaikia kuzishau-ri akili zenye kufikiria na nafsi zenye kutafuta haki, ili ziweze kufikia kwenye haki ambayo inatolewa na Kambi ya Ahlul-Bait ulimwengu

mzima, ndani ya zama ambazo akili inaerevuka na nafsi na roho zinabore– ka kwa kasi ya pekee.

Ni lazima tugusie kuwa mfululizo huu wa tafiti hizi umeandaliwa na Kamati maalumu toka jopo la wanachuoni watukufu, hivyo tunatoa shuku– rani njema kwa hawa wote na kwa wasomi na wahakiki kwa kila mmoja miongoni mwao kwa kupitia sehemu ya tafiti hizi na kutoa mchango wao wa thamani kuhusu tafiti hizi.

Na sote tunategemea na kutaraji kuwa tutakuwa tumetoa kile tulichoki– weza katika juhudi za kutekeleza baadhi ya wajibu tulionao mbele ya ujumbe wa Mtukufu Mola Wetu Mlezi ambaye alimtuma Mtume Wake na uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi dhidi ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlu–Bait

Kitengo cha utamaduni

Source URL: <https://www.al-islam.org/sw/imam-mahdi-katika-usunni-na-ushia/neo-la-jumuiya-0>